# HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO(CMT)

**KILICHOFANYIKA TAREHE 11.10.2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA MJI**

**MAHUDHURIO YA WAJUMBE**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Bw.Josephat W.Kayombo | -Kaimu Mkurugenzi wa Mji | -Mwenyekiti |
| 2. Bw.Laurent M.Kapimpiti | -Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi | -Katibu |
| 3. Bw.Victor Magafu | -Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji | -Mjumbe |
| 4. Bw.Abdul S.Mbwana | -Mkuu wa Idara ya Mipangomiji,Ardhi na Maliasili | -Mjumbe |
| 5. Bw.Engelbert Maro | -Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | -Mjumbe |
| 6. Bi.Rita J.Kamenya | -Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii | -Mjumbe |
| 7. Bw.Boniface Mwasandube | -Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara | -Mjumbe |
| 8. Bw.Freza B.Mapunda | -Mratibu waTASAF | -Mjumbe |
| 9. Bi.Pamela S.Ijumba | -Mkuu wa Idara ya Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika | -Mjumbe |
| 10.Mwl.Nisile Burton | -Kny.Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari | -Mjumbe |
| 11.Eng.Dickson Kisenime | -Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi | -Mjumbe |
| 12.Bi.Elisa Mwambene | -Kny.Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ugavi | -Mjumbe |
| 13.Adv.Frank Sikalengo | -Kny;Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria | -Mjumbe |
| 14.Dkt.Enock Mwambalaswa | -Mkuu wa Idara ya Afya | -Mjumb |
| 15.Mwl.Wilson Mtafya | -Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi | -Mjumbe |
| 16.Bw.Lusajo N.Mwaluksa | -Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi | -Mjumbe |
| 17.Bw.Eddie J.Mhelela | -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA | -Mjumbe |
| 18.Bw.Marco J.Ipini | -Kny;Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira | -Mjumbe |
| 19.Bw.Bernard R.Kishamba | -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi | -Mjumbe |
| 20.Bw.William Maganga | -Afisa Habari na Mahusiano | -Mjumbe |
| 21.Bw.Charles M.Mazengo | -Afisa Biashara | -Mjumbe |

**WATAALAM WASIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1.Bw. Josephat Magoto | -Afisa Tarafa Tunduma | - Kwa taarifa |

**SEKRETARIETI**

1.Bw. Majenje Laison -Mwandishi wa vikao vya Halmashauri ya Mji

**AGENDA ZILIZOJADILIWA**

1.Kufungua kikao.

2.Kuridhia agenda za kikao.

3.Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 15.09.2021.

4.Yatokanayo na kikao cha tarehe 15.09.2021 na utekelezaji wake.

5.Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri ya Mji kuishia tarehe 30 Septemba 2021.

6.Taarifa ya utekelezaji na ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021).

7.Kupokea na kujadili taarifa za na Vitengo katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021)

- Kitengo cha Manunuzi
- Kitengo cha Sheria
- Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
- Idara ya Utawala na Raslimali Watu.

8. Taarifa ya Magari,Pikipiki na Mafuta.

9. Mapendekezo ya uboreshaji wa Mfumo wa utoaji wa Mikopo yenye tija kwa Vikundi.

10. Mapendekezo ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Majengo ya Shule kwa Ramani ya Ghorofa.

11.Mkakati wa Usimamizi wa tozo za Taka ngumu katika Kata **3** na Majaribio.

12.Mapokezi ya fedha kiasi cha Shs.**1,880,000,000.00** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya Mradi wa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19

13.Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti

14.Kufunga kikao.

**MUHT. NA.TTC/CMT/01/10/2021 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa mahudhurio mazuri. Aliwasihi kuelekeza fikra zao kikaoni na kujadili agenda zilizopo kwa umakini.Kisha alifungua kikao mnamo saa **04:10** asubuhi.

**MUHT.NA.TTC/CMT/02/10/2021 KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO**

Agenda za kikao ziliwasilishwa na kuridhiwa na wajumbe kwa pamoja.

**MUHT.NA.TTC/CMT/03/10/2021 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 15.09.2021.**

Muhtasari wa kikao cha kawaida cha Wakuu wa Idara na Vitengo (CMT)kilichofanyika tarehe **15.09.2021** ulisomwa na wajumbe na kuuthibitisha.Kisha Mwenyekiti aliusani kuashiria kwamba tayari ni kumbukumbu halali ya Halmashauri ya Mji Tunduma.

**MUHT.NA.TTC/CMT/04/10/2021 YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 15.09.2021 NA UTEKELEZAJI WAKE.**

Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya kikao cha kawaida cha Wakuu wa Idara na Vitengo (CMT) kilichofanyika tarehe **15.09.2021** iliwasilishwa na kujadiliwa na wajumbe kama ifuatavyo;

**Azimio na 1:**Kwamba Timu ya wataalam ifanye ufuatiliaji na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizopo katika Soko la Tazara na kuwasilisha mapendekezo ya namna ya kuliboresha ili kuhakikisha linafanya kazi kama chanzo cha mapato ya Halmashauri ya Mji.Aidha kazi ifanyike ndani ya siku 7 kuanzia leo tarehe **15.09.2021**

**Utekelezaji;** Ilielezwa kwamba Kamati inaendelea kutafuta ufumbuzi wa changamoto za Soko la Tazara na inaendela kukutana na viongozi wa block zote ili kupata maoni yao na kukutana na wafanyabiashara wa kila vyumba kujua changamoto zao za kutoendelea na ujenzi Taarifa ya awali iliambatishwa.

**Azimio namba 2:**Kwamba iandaliwe Regista ya Madeni ambayo itatunzwa na Kitengo cha Manunuzi (PMU). Aidha kila Idara ihakikishe inakuwa na Regista ya Madeni katika Idara husika.

**Utekelezaji**:Ilielezwa kwamba agizo limezingatiwa tayari Regista ya madeni imeandaliwa format maalum itawasilishwa kwenye kikao cha CMT cha tarehe **11.10.2021** ili kuridhiwa na kugawiwa kwa kila Mkuu wa Idara.

**Azimio namba 3.** Kwamba ufanyike uhakiki wa nyaraka za madai ya Mzabuni wa Mafuta Panone ili kujiridhisha na madai yake.

**Utekelezaji:**Ilielezwa kwamba agizo limezingatiwa. Tayari nyaraka zimetafutwa na zimepatikana za Tsh. **3,123,000.00** ndizo zilizoonekana.

**Azimio namba 4:** Kwamba mapato yaliyoingizwa katika Akaunti ya Amana ambayo ni mauzo katika Duka la Dawa yahamishiwe kwenye Akaunti husika.

**Utekelezaji:** Agizo limetekelezwa kiasi cha Shs.**465,724.00** za Duka la dawa ziliingizwa katika akaunti ya amana zimesharejeshwa katika akaunti ya makusanyo ya Halmashauri tarehe **29.09.2021.**

**Azimio namba 5:** Kwamba ateuliwa Meneja wa Duka la Dawa mwenye taaluma ya Dawa kutoka Idara ya Afya .

**Utekelezaji:** Kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu amependekezwa Dr.Godfrey Ngallunga-Tabibu awe Meneja.

**Azimio namba 6:** Kwamba ili kudhibiti upotevu wa mapato Mifumo ya GoTHOMIS ifungwe katika Vituo vyote vya kutolea huduma za Afya na fedha kiasi cha Shs.**18,000,000.00** itumike katika kununua Kompyuta na mrejesho utolewe tarehe **20/09/2021.**

**Utekelezaji:**Ilielezwa kwamba agizo limetekelezwa. Dokezo la kununua Komputa **18** UPS,Server na Cable wire limeandikwa tararibu za manunuzi zinaendelea.

Wajumbe walipongeza kwa utekelezaji wa agizo hili kwani itasaidia katika kuongeza mapato ya Halmashauri.

**MUHT.NA.TTC/CMT/05/10/2021 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021**

Kaimu Mweka Hazina aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri ya Mji Tunduma katika kipindi cha kuishia tarehe 30 Septemba 2021.

Ilielezwa kwamba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Mji wa Tunduma imeidhinishiwa Makisio ya kukusanya mapato ya ndani na kupokea fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wahisani wa Maendeleo Jumla ya **TZS. 31,644,378,303.00** kutoka vyanzo mbalimbali kama zinavyoonekana kwenye Jedwali lifuatalo:-

JEDWALI NA. 1: MUHTASARI WA MAKISIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

| NA. | MAELEZO | KIASI (TSHS) |
|---|---|---|
| 1 | Fedha za makusanyo ya mapato ya ndani | 5,635,690,500.00 |
| 2 | Fedha za ruzuku ya serikali kwa ajili ya Matumizi mengineyo | 792,117,455.00 |
| 3 | Fedha za ruzuku ya Miradi ya Maendeleo na wa Wahisani | 12,781,853,000.00 |
| 4 | Fedha za ruzuku kwa ajili ya Mishahara | 12,434,717,348.00 |
| | **JUMLA KUU YA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022** | **31,644,378,303.00** |

Mhe:Mwenyekiti, kwa kipindi cha Mwezi Septemba,2021 Halmashauri imefanikiwa kukusanya mapato ya ndani na kupokea fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu na wahisani kiasi cha **TZS.1,917,853,576.71** na Jumla ya mapato kuanzia Julai hadi Septemba,2021 ni **TZS. 5,295,607,273.33** ambayo ni sawa na asilimia **16.75%** ya makisio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**JEDWALI NA.2: MUHTASARI WA MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI NA MAPOKEZI YA FEDHA ZA RUZUKU YA SERIKALI KUU NA WAHISANI KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA,2021**

| MAELEZO | MAKISIO YA MWAKA WA FEDHA 2021/22 | MAPATO TULIYOKUSANYWA AGOSTI,2021 | MAPATO TULIYOKUSANYWA KWA MWEZI SEPTEMBA,2021 | MAPATO TULIYO KUSANYA JULAI-SEPTEMBA,2021 | TOFAUTI KATI YA MAKISO NA MAKUSANYO | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Fedha za makusanyo ya Mapato ya ndani | 5,635,690,500.00 | 1,400,739,264.01 | 802,180,417.49 | 2,202,919,681.50 | 3,432,770,818.50 | 39.09 |
| Fedha za Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida | 792,117,455.00 | 225,946,083.30 | 56,472,166.60 | 282,418,249.90 | 509,699,205.10 | 35.65 |
| Fedha za Ruzuku kwa ajili ya Mishahara (PE) | 12,434,717,348.00 | 1,694,405,000.00 | 859,996,100.00 | 2,554,401,100.00 | 9,880,316,248.00 | 20.54 |
| Fedha za Ruzuku za Miradi ya Maendeleo | 12,781,853,000.00 | 56,663,349.31 | 228,374,574.51 | 285,037,923.82 | 12,496,815,076.18 | 2.23 |
| **JUMLA KUU** | **31,644,378,303.00** | **3,377,753,696.62** | **1,947,023,258.60** | **5,324,776,955.22** | **26,319,601,347.78** | **16.83** |

Mhe:Mwenyekiti,Katika kipindi cha Mwezi Septemba,2021 Halmashauri ilipokea fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu kiasi cha **TZS. 1,115,673,159.22** Kwa ajili ya Ulipaji wa Mishahara ya watumishi wa Ruzuku na Fedha za matumizi ya kawaida kwa ajili ya uendeshaji wa Mitihani wa Darasa la saba.Mchanganuo wa maapokezi hayo ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini:-

**JEDWALI NA:3 MAPOKEZI YA FEDHA ZA RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA,2021**

| S/NA | MAELEZO YA FEDHA | FEDHA |
|---|---|---|
| i | Mishahara ya watumishi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu | 859,996,100.00 |
| ii | Ruzuku ya matumizi ya kawaida (Other charges) | 56,472,166.60 |
| iii | Elimu Bila Malipo | 153,268,912.89 |
| iv | MIRADI YA WALTEREED | 47,724,813.40 |
| | **JUMLA KUU TZS.** | **1,117,461,992.89** |

Mhe:Mwenyekiti,Katika kipindi cha Mwezi Mitatu kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kuanzia tarehe 01.07.2021 hadi tarehe 30.09.2021 Halmashauri ilikuwa na Malengo ya kukusanya mapato ya ndani na kupokea fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu kiasi cha **TZS. 8,380,735,450.75** Kati ya malengo hayo Halmashauri ilifanikuwa kukusanya na kupokea fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu kiasi cha **TZS. 5,295,607,273.33** sawa na **63.19%** ya malengo ya Makusanyo na Mapokezi kwa mwaka wa fedha 2020/21 kama inavyoonekana kwenye Jedwali lifuatalo:-

**JEDWALI NA.4: MUHTASARI WA MALENGO YA MAKUSANYO NA MAPATO HALISI YA MAPATO YA NDANI NA MAPOKEZI YA FEDHA ZA RUZUKU KWA KIPINDI CHA MIEZI MITATU KUANZIA MWEZI JULAI,2021 HADI 30 SEPTEMBA,2021**

| MAELEZO | LENGO LA MAKUSANYO LA MIEZI MITATU | MAPATO TULIYOKUSANYWA JULAI - AGOSTI,2021 | MAPATO TULIYOKUSANYWA KWA MWEZI SEPTEMBA,2021 | MAPATO TULIYOKUSANYA JULAI-SEPTEMBA,2021 | TOFAUTI YA MALENGO NA MAKUSANYO | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Fedha za makusanyo ya vyanzo vya ndani | 1,878,563,500.00 | 1,400,739,264.01 | 802,180,417.49 | 2,202,919,681.50 | -324,356,181.50 | **117.27** |
| Fedha za Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida | 264,039,151.67 | 225,946,083.30 | 56,472,166.60 | 282,418,249.90 | -18,379,098.23 | **106.96** |
| Fedha za Ruzuku kwa ajili ya Mishahara | 3,108,679,337.00 | 1,694,405,000.00 | 859,996,100.00 | 2,554,401,100.00 | 554,278,237.00 | **82.17** |
| Fedha za Ruzuku za Miradi ya Maendeleo | 3,195,463,250.00 | 56,663,349.31 | 228,374,574.51 | 285,037,923.82 | 2,910,425,326.18 | **8.92** |
| **JUMLA KUU** | **8,446,745,238.67** | **3,377,753,696.62** | **1,947,023,258.60** | **5,324,776,955.22** | **3,121,968,283.45** | **63.04** |

Kama Jedwali hapo juu linavyoonekana kuwa hatukuweza kufikia malengo ya mapokezi ya fedha kutoka Serikali Kuu kwa sababu bado hatujapokea fedha za Miradi ya Maendeleo katika robo ya kwanza

**MATUMIZI:**

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri imekisia kutumia kiasi cha **TZS.31,644,378,303** kutoka vyanzo mbalimbali, Aidha kwa Mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ilibakiwa na bakaa kiasi cha **TZS.112,042,729.95** Fedha hizi zilizosalia zimeunganishwa kwenye makisio ya matumizi ya mwaka huu wa fedha ili ziweze kutumika hivyo kufanya makisio ya Matumizi kuongezeka kutoka **TZS. 31,644,378,303.00** Hadi kufikia kiasi cha **TZS.31,756,421,032.95** kama Jedwali lifuatavyo linavyoonekana:-

**JEDWALI NA. 5 :MUHTASARI WA SURA YA MATUMIZI YA MWAKA 2021/2022**

| MAELEZO | MAKISIO 2021/2022 |
|---|---|
| Salio Anzia la mwaka 2020/2021 | 112,042,729.95 |
| Makusanyo ya vyanzo vya ndani | 5,635,690,500.00 |
| Ruzuku ya Serikali kuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida (OC) | 792,117,455.00 |
| Ruzuku ya Serikali kuu kwa ajili ya Mishahara | 12,434,717,348.00 |
| Fedha za Miradi ya Maendeleo na wahisani | 12,781,853,000.00 |
| **JUMLA KUU YA BAJETI YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022** | **31,756,421,032.95** |

Kwa kipindi cha mwezi Septemba,2021 Halmashauri imetumia kiasi cha **TZS.1,593,491,897.55** na Jumla ya matumizi kuanzia **01.07.2021 hadi 30.09.2021** kufikia **TZS. 4,013,270,473.52** ikiwa ni sawa na asilimia **12.60%** ya makisio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kama Jedwali lifuatalo linavyoonekana:-

**JEDWALI NA. 6: MUHTASARI WA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA KUISHIA 30.SEPTEMBA.2021**

| MAELEZO | MAKISIO YA MWAKA 2021//2022 | MATUMIZI KUANZIA JULAI HADI AGOSTI,2021 | MATUMIZI HALISI MWEZI SEPTEMBA, 2021 | MATUMIZI HALISI MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA,2021 | TOFAUTI YA MAKISIO NA MATUMIZI | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bakaa | 112,042,729.95 | - | 100,602,880.00 | 100,602,880.00 | 11,439,849.95 | 90 |
| Matumizi ya kawaida kwa Fedha za Mapato ya Ndani | 3,024,645,250.00 | 353,132,426.66 | 284,365,154.66 | 637,497,581.32 | 2,387,147,668.68 | 21 |
| Miradi ya Maendeleo kwa Fedha za Mapato ya Ndani | 2,611,045,250.00 | 158,057,000.00 | 224,581,450.00 | 382,638,450.00 | 2,228,406,800.00 | 15 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya kawaida (OC) | 792,117,455.00 | 157,520,800.00 | 7,688,400.00 | 165,209,200.00 | 626,908,255.00 | 21 |
| Ruzuku ya Serikali kuu kwa ajili ya Mishahara | 12,434,717,348.00 | 1,694,405,000.00 | 859,996,100.00 | 2,554,401,100.00 | 9,880,316,248.00 | 21 |
| Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo na wahisani | 12,781,853,000.00 | 56,663,349.31 | 115,768,912.89 | 172,432,262.20 | 12,609,420,737.80 | 1 |
| **JUMLA KUU** | **31,756,421,032.95** | **2,419,778,575.97** | **1,593,002,897.55** | **4,012,781,473.52** | **27,743,639,559.43** | **12.6** |

Kwa kipindi cha Miezi Mitatu kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kuanzia tarehe 01.07.2021 hadi tarehe 30.09.2021 Halmashauri ilikuwa na Malengo ya kutumia kiasi cha **TZS. 7,939,105,258.24** Kati ya malengo hayo Halmashauri ilifanikuwa kutumia kiasi cha **TZS. 4,013,270,473.52**sawa na **50.55%** ya malengo la Makusanyo na Mapokezi kwa mwaka wa fedha 2021/22 kama inavyoonekana kwenye Jedwali lifuatalo:-

**JEDWALI NA. 7: MUHTASARI WA MALENGO YA MATUMIZI NA MATUMIZI HALISI KWA KIPINDI CHA MIEZI MITATU KUANZIA MWEZI JULAI,2021 HADI SEPTEMBA,2021**

| MAELEZO | LENGO LA MATUMIZI YA MIEZI MITATU | MATUMIZI HALISI JULAI HADI AGOSTI,2021 | MATUMIZI HALISI MWEZI SEPTEMBA,2021 | MATUMIZI HALISI JULAI-SEPTEMBA,2021 | TOFAUTI YA LENGO NA HALISI | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bakaa/Salio | 28,010,682.49 | - | 100,602,880.00 | 100,602,880.00 | -72,592,197.5125 | 359 |
| Matumizi ya kawaida kwa Fedha za Mapato ya Ndani | 756,161,312.50 | 353,132,426.66 | 284,365,154.66 | 637,497,581.32 | 118,663,731.1800 | 84 |
| Miradi ya Maendeleo kwa Fedha za Mapato ya Ndani | 652,761,312.50 | 158,057,000.00 | 224,581,450.00 | 382,638,450.00 | 270,122,862.5000 | 59 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya kawaida (OC) | 198,029,363.75 | 157,520,800.00 | 7,688,400.00 | 165,209,200.00 | 32,820,163.7500 | 83 |
| Ruzuku ya Serikali kuu kwa ajili ya Mishahara | 3,108,679,337.00 | 1,694,405,000.00 | 859,996,100.00 | 2,554,401,100.00 | 554,278,237.0000 | 82 |
| Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo na wahisani | 3,195,463,250.00 | 56,663,349.31 | 115,768,912.89 | 172,432,262.20 | 3,023,030,987.8000 | 5 |
| **JUMLA KUU** | **7,939,105,258.24** | **2,419,778,575.97** | **1,593,002,897.55** | **4,012,781,473.52** | **3,926,323,784.72** | **50.54** |

**CHANGAMOTO KATIKA UKUSANYAJI WA MAPATO**

1. Mwamko mdogo wa wananchi katika uchangiaji wa huduma za afya

2.Uwepo wa ugonjwa COVID 19 umeathiriki uchumi wa wafanyabiashara hivyo kuathirika katika ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri.

**UTATUZI WA CHANGAMOTO KATIKA UKUSANYAJI WA MAPATO**

1. Kuunda kikosi kazi cha uhamasishaji wa wananchi kujiunga na CHF iliyoboreshwa.

2.Elimu imeendelea kutolewa kwa wafanyabiashara ili biashara zao ziendelee huku wakiendelea kujinga na COVID 19.

**Mjadala.**

Wajumbe walishauri kasi ya ufutiliaji iongezwe katika vyanzo vya mapato ambavyo makusanyo yake bado hayaridhishi hususani vyanzo ya sekta ya Afya.

Aidha walipongeza Idara ya Fedha na Biashara kwa kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato ambapo kwa mwez Septemba rekodi imevunjwa kwa kukusanya zaidi ya Shs.**800,000,000.00**

Wajumbe waliipokea taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri ya Mji Tunduma kuishia tarehe **30** Septemba **2021.**

**MUHT.NA.TTC/CMT/06/10/2021 TAARIFA YA UTEKELEZAJI NA UFUATILIAJI WA MIRADI KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI HADI SEPTEMBA 2021)**

Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021).

Ilielezwa kwamba katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ya Mji wa Tunduma ilipang kupokea na kutumia jumla ya Shs.**13,926,466,450** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutok vyanzo mbalmbal. Hadi kufikia mwezi Septemba2021 Halmashauri imepokea jumla y S**h.1,169,169,033.39** sawa na asilimia **9.23** kutoka vyanzo mbalimbali. Mapato na matumizi ya fedha z miradi ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

| NA | CHANZO CHA FEDHA | MAKISIO | MAPOKEZI AGOSTI, 2021 | MAPOKEZI YA SEPTEMBA, 2021 | JUMLA YA MAPOKEZI JULAI-SEPTEMBA, 2021 | TOFAUTI YA MAKISIO NA MAPOKEZI HALISI | FEDHA ILIYOTUMIIA JULAI - SEP 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | (Mfuko wa Afya) Basket Fund | 28,342,200 | | | | 28,342,200.00 | |
| 2 | UNICEF | 229,763,000 | | | | 229,763,000.00 | |
| 3 | CDCF | 35,000,000 | | | | 35,000,000.00 | |
| 4 | Ruzuku ya ujenzi wa Hospitali | 1,000,000,000 | | | | 1,000,000,000.00 | |
| 5 | Free Education | 837,758,000 | | 115,768,912.89 | 115,768,912.89 | 721,989,087.11 | 115,768,92.89 |
| 7 | P4R | 693,163,000 | | | | 693,163,000.0 | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8 | Walter Reed | 204,589,000.00 | | 46,724,813.39 | 46,724,813.39 | 157,864,186.61 | |
| | Ujenzi wa Miradi Mkakati - Maegesho ya Malori | 400,000,000.00 | | | | 400,000,000.00 | |
| 9 | Global Fund TB & Malaria, HIV | 29,159,000 | | | | 29,159,000.00 | |
| 10 | Ujenzi wa Miradi Mkakati-Stendi | 600,000,000 | | | | 600,000,000.00 | |
| 11 | Ujenzi wa jengo la Utawala | 1,000,000,000 | | | | 1,000,000,000.00 | |
| 12 | Ukamilishaji wa madarasa ya Msingi | 112,500,000 | | | | 112,500,000.00 | |
| 13 | Ukamilishaji wa madarasa ya Sekondri | 112,500,000 | | | | 112,500,000.00 | |
| 14 | Ununuzi wa vifaa tiba | 500,000,000 | | | | 500,000,000.00 | |
| 15 | Ujenzi wa vyumba vya madarasa LANES | 64,000,000 | | | | 64,000,000.00 | |
| 16 | NTD | 15,547,000.00 | | | | 15,547,000.00 | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Zahanati ya Nyerere | 0 | | | | 50,000,000.00 | |
| 18 | Ujenzi wa Zahanati ya Niumba | 50,000,000.00 | | | | 50,000,000.00 | |
| 19 | Mpango wa kuinua Elimu - SEQUIP | 5,209,900,000.00 | | | | 5,209,900,000.00 | |
| 20 | Miradi ya huduma za Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira - SWASH | 37,000,000.00 | | | | 37,000,000.00 | |
| 21 | Mfuko wa Jimbo | 35,000,000 | | | | 35,000,000.00 | |
| | Mapato ya ndani | 2,682,245,250 | | | 1,122,444,220.00 | 1,559,801,030.00 | 417,744,2[illegible]0.00 |
| | **JUMLA MUU** | **13,926,466,450.00** | **0.00** | **162,493,726.28** | **1,284,937,946.28** | 12,641,528,503.72 | **533,513,1[illegible]2.89** |

Wajumbe waliipokea taarifa ya utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021).

**MUHT.NA.TTC/CMT/07/10/2021 KUPOKEA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KUTOKA IDARA NA VITENGO KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI HADI SEPTEMBA 2021).**

- **TAARIFA YA KITENGO CHA MANUNUZI**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi aliwasilisha taarifa ya Kitengo cha Manunuzi katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba 2021.

Ilielezwa kwamba kwa Mujibu wa Sheria ya Manunuzi Na.7 ya Mwaka 2011 pamoja na kanuni zake za Mwaka 2013,Taarifa ya Manunuzi yaliyofanyika katika kipindi cha robo ya

Utawala ili ijadiliwe.

Aidha katika kipindi tajwa hapo juu, Halmashauri imetekeleza Manunuzi mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao;

| Na. | AINA YA MANUNUZI | GHARAMA (TSH) |
|---|---|---|
| 1. | Manunuzi ya Bidhaa (Goods) | 321,551,635.83 |
| 2 | Manunuzi ya Huduma za Kitalaamu (Consultancy Services) | 00 |
| 3. | Huduma (NonConsultancy Service) | 16,985,200.00 |
| 4 | Kazi (Works) | 00 |
| | **JUMLA KUU** | **338,536,835.83** |

Mchanganuo wa matumizi kwa kila idara/Kitengo ni kamaifuatavyo;

| NA. | IDARA/KITENGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | UTAWALA | 83,665,000.23 |
| 2 | AFYA TIBA | 125,718,975.6 |
| 3 | FEDHA NA BIASHARA | 1,900,000.00 |
| 4 | USAFI NA MAZINGIRA | 41,042,000.00 |
| 5 | UGAVI | 3,990,000.00 |
| 6 | ELIMU MSINGI | 38,751,860.00 |
| 7 | UJENZI | 1,235,000.00 |
| 8 | IMPREST | 2,500,000.00 |
| 9 | MRADI WA TOFALI | 40,920,000.00 |
| | **JUMLA KUU** | **339,722 ,835.83** |

Mchanganuo wa Manunuzi hayo kwa kila Idara na Vitengo uliambatishwa.

Wajumbe waliipokea taarifa ya Kitengo cha Manunuzi katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021).

- **TAARIFA YA KITENGO CHA SHERIA**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria aliwasilisha taarifa ya utekekelezaji wa shughuli za Kitengo katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021).

Ilielezwa kwamba Kitengo cha Sheria kimetekeleza majukumu yake katika kipindi cha robo ya kwanza katika mwaka wa fedha **2021/2022** kama ifuatavyo;

Hadi kufikia tarehe **30/09/2021** Halmashauri inakabiliwa na kesi nne(**4)** zinazotokana na migogoro ya ya Ardhi yenye thamani ya **Shs.3,146,400,000/=**

Ilielezwa kwamba Halmashauri ya Mji Tunduma inakabiliwa na kesi mbili (2) zinazotokana na migogoro ya Mawakala yenye thamani ya ya **Shs. 77,610,186**.**00**

Halmashauri ya Mji Tunduma inakabiliwa na kesi **37** zinazotokana na Madeni ya mikopo ya vikundi yenye thamani ya **Shs**.**251,487,239**.**00**

Hata hivyo Halmashauri imeshinda kesi moja ya mgogoro na Wakala Rufaa **Na.3/2020 k**ati ya Lusungo Investment Dhidi ya Halmashauri ya Mji Tunduma kupinga kutolipa hasara ya **Shs.75,641,150.00**

Hata hivyo Halmashauri inahitaji msaada wa Wakili Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kusaidia kesi ya **Vadeen Co. Ltd dhidi ya Halmashauri Ya Mji Tunduma Rufaa na 22/2021** ambayo Halmashauri inatarajia kukata rufaa kupinga maamuzi ya Mahakama Kuu.

**TAARIFA ZA KESI ZA HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA ROBO YA KWANZA 2021/2022**

| NA. | WAHUSIKA NA NAMBA YA SHAURI | MAHAKAMA | MADAI | MSIMAMIZI WA KESI | MAENDELEO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Lusungo investment Dhidi ya Halmashauri ya Mji Tunduma rufaa namba 3/2020 | Mahakama Kuu Mbeya | Halmashauri imekata rufaa kwa kupinga maamuzi yaliyo tolewa na mahakama ya wilaya momba ikiwa inadai tshs. **41,100,000/=** | Wakili wa serikali Halmashauri ya Mji Tunduma | Hukumu imesomwa tarehe 30/09/2021 Halmashauri imeshinda kesi |
| 2. | Halmashauri ya mji Tunduma dhidi ya Kalebu Asajile na wengine wanne (4) maombi namba 119/2020 | Baraza la Wilaya la Ardhi Mbeya | Uvamizi wa eneo la Halmashauri lililopo Kata ya Mpande ekari 79 lenye thamani ya Tshs. **46,400,000/=** | Wakili wa Serikali Halmashauri ya mji tunduma | Kesi itasikilizwa tarehe 13/10/2021 |
| 3. | Jamal Mohamed Ahamed dhidi ya | Mahakama Kuu Mbeya | Uvamizi wa eneo la mmiliki wa asili | Mwanasheria Halmashauri ya | Kesi itatajwa tarehe |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Msongole na Halmashauri ya Mji Tunduma kesi namba 21/2021 | | | | |
| 4. | Halmashauri ya Mji Tunduma dhidi ya Vadeen Co. Ltd | Mahakama Kuu | Halmashuari imekata rufaa kwa kupinga maamuzi yaliyo tolewa na Mahakama ya Wilaya Momba kulipa Tshs. 48,650,000/= | Mwanasheria Halmashauri ya Mji Tunduma | Kesi itatajwa tarehe 26/10/2021 |
| 5. | Panone Co Ltd dhidi ya Halmashauri ya Mji Tunduma na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kesi namba 05/2021 | Mahakama Kuu Mbeya | Madai yaliyotokana na deni la huduma ya mafuta kwa Halmashauri Tshs. **28,960,186/=** | Wakili wa Serikali Halmshauri ya Mji Tunduma na Wakili Mkuu wa Serikali kanda ya Mbeya | Kesi itasikilizwa tarehe 11/11/2021 |
| 6. | Harold Siame dhidi ya Halmashauri ya Mji Tunduma maombi namba 2/2021 | Baraza la Ardhi Wilaya la Mbozi | Kupinga kuondoka kwenye viwanja alivyovamia kudai fidia ya tshs. **100,000,000/=** | Wakili wa Serikali Halmshauri ya Mji Tunduma na Wakili Mkuu wa Serikali kanda ya Mbeya | Kesi itasikilizwa tarehe 08/10/2021 |
| 7. | Roga Ramadhani na wengine 34 dhidi ya Halmashauri ya Mji Tunduma kesi namba 22/2019 | Mahakama Kuu Mbeya | Wananchi wanadai fidia kwa nyumba zilizo bomolewa kupisha upanuzi wa mpaka wa Tanzania na Zambia Tshs. **3,000,000,000/=** | Wakili wa Serikali Halmashauri ya mji Tunduma na wakili mkuu wa serikali kanda ya mbeya | Kesi itasikilizwa tarehe 08/10/2021 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Mwafwanga dhidi ya Halmshauri ya Mji Tunduma na wengine wawili (02) kesi namba 54/2021 | Kuu Mbeya | | wa halmashauri | tarehe 08/10/2021 |

Wajumbe waliipokea taarifa ya Kitengo cha Sheria katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021).

- **TAARIFA YA KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI**

Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani aliwasilisha taarifa ya Ukaguzi wa Ndani katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021).

Ilielezwa kwamba Kitengo cha Ukaguzi kinafanya kazi zake kwa kuzingatia sheria ya fedha (Finance Act) No.9 ya mwaka 1982 kifungu kidogo No 45(1) na Mwongozo wa fedha *Local Government Financial Memorandum ya mwaka 2009* Agizo Na.13-14 pamoja na Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani (*Local Government Audit Manual*) wa mwaka 2013 na 2016,Mwongozo wa Ukaguzi wa miradi (Construction Projects Audit Manual) wa November 2015,Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) pamoja na kanuni zake za mwaka 2013.

Uwasilishaji wa taarifa hii ni kwa mujibu wa memorandum ya fedha oda namba 12(5)(a-g ) ya mwaka 2009.

**UTEKELEZAJI WA HOJA ZA NYUMA**

Katika utekelezaji wa hoja za nyuma mpaka sasa hoja moja **(1 )** bado haijafungwa ambayo ni

:

| Ripoti | Namba ya hoja | Hoja |
|---|---|---|
| Robo ya nne | 9.1 | Fedha ambazo hazijarejeshwa za vikundi vya wanawake na vijana Tshs.**191,889,267.00** kwa kipindi cha mwaka 2017/2018,2018/2019 |

| | | |
|---|---|---|
| | | Mpaka sasa marejesho ya Tshs.**169,755,867.00** hayajarejeshwa |

**UTEKELEZAJI WA MAJIBU YA HOJA ROBO YA KWANZA**

Katika robo ya kwanza kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2021 jumla ya hoja **14** zilitolewa katika robo husika. Katika utekelezaji wa majibu ya hoja, jumla ya hoja **09** zilifungwa, hoja **03** hazijafungwa, na hoja **02** uhakiki utafanyika robo ijayo Mchanganuo wa kila hoja umeambatanishwa kwenye jedwali ndani ya taarifa hii.

Baada ya kuwasilisha taarifa wajumbe waliipokea na kukubaliana ziwasilishwe ambazo bado hazijafungwa. Hoja hizo ni pamoja na;-

| **Na.** | **Hoja** |
|---|---|
| 1.6 | Kutokuwepo kwa Regista ya Madeni |
| 2.2 | Malipo kwa watoa huduma bila kutoa risiti za EFD |
| 3.1 | Halmashauri kutopata kodi kutokana na mauzo ya viwanja |

Mwenyekiti alisisitiza kuhusu kukamilisha zoezi la kuwasilisha majibu ya hoja katika Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani ili kabla ya kikao cha Kamati ya Ukaguzi hoja ziwe zimejibiwa na kufungwa.

Wajumbe waliipokea taarifa ya Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021).

**-TAARIFA YA IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI**

Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi aliwasilisha taarifa ya Idara katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021).

ya Idara ya Maji na Idara ya Ardhi na Mipangomiji kuhamia Serikali Kuu. Kutokana na maandalizi ya Ikama ya Watumishi na bajeti ya Mishahara kwa mwaka 2020/2021,

Halmashauri ina mahitaji ya Watumishi **1,297** Waliopo ni **1,077**, Upungufu ni 220 Katika Ikama ya Mwaka 2019/2020 Halmashauri iliidhinishiwa nafasi za Ajira Mpya 246 ambapo tumepata watumishi ajira mpya Elimu Msingi **26**, Elimu Sekondari **11** na Afya **08** hivyo kuwa na jumla ya watumishi **45** ambao wamesaidia kwa kiasi kupunguza pengo la watumishi katika Halmashauri ya Mji Tunduma .

**KUSHUGHULIKIA MALIPO YA MISHAHARA**

Idara kwa kipindi cha taarifa imeweza kuandaa mishahara ya watumishi kwa kushirikiana na Idara zote zenye kasma za Mishahara kama ifuatavyo;

| Na. | Kipindi cha Malipo ya Mshahara (Septemba 2021) | Idadi ya Watumishi | Kiasi cha Mshahara kilichoidhinishwa | Idadi ya Waliosimamishiwa/Kupunguziwa Mishahara | Kiasi cha Fedha Waliosimamishiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Septemba | **1,076** | **860,485,100** | **02** | **305,565.72** |

**Changamoto**

1. Ukosefu wa jengo la Ofisi la Halmashauri. Hali hii inapelekea kupanga jengo na kutumia gharama kubwa kwa mwaka **40,000,000/=** kama pango ingawa pia halitoshelezi kwa mahitaji ya vyumba vya ofisi. Tunaishukuru Serikali kwa kuidhinisha kwenye bajeti ya mwaka 2020/2021 kiasi cha Shs. **750,000,000** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi.

2. Upungufu wa Watumishi katika taasisi. Halmashauri tangu ianzishwe Julai Mosi, 2015 haijapata kuajiri watumishi wa kutosha katika sekta zote. Kwa sasa tuna upungufu wa watumishi **265** ambapo sekta zenye uhitaji mkubwa ni, Elimu, Afya, Kilimo na Fedha na Biashara. Kwenye Ikama ya mwaka 2019/2020 Serikali imeidhinisha nafasi za ajira mpya **130**, kibali cha kuajiri kikitolewa itasaidia kupunguza pengo lililopo.
3. Vifaa vya usafiri. Kukosekana kwa vifaa vya usafiri kwa idadi toshelezi. Magari ya Halmashauri ni machache sana ukilinganisha na wigo wa majukumu. Ofisi itaendelea kutenga Bajeti ili kuwezesha ununuzi wa magari kwa lengo la kupunguza uhaba uliopo.

Wajumbe waliipokea taarifa ya Idara ya Utawala na Utumishi katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba 2021).

**MUHT.NA.TTC/CMT/08/10/2021 TAARIFA YA MAGARI,MAFUTA NA PIKIPIKI**

Ilielezwa kwamba Halmashauri ya Mji Tunduma ina jumla ya magari kumi na saba (17) na pikipiki ishirini na saba (27). Kati ya magari hayo 17 magari 10 yanafanya kazi na yapo kwenye hali nzuri, magari 2 yapo karakana ya za TEMESA (STL 1644 Temesa Mbeya na Canter FE517BD-52 lipo TEMESA Songwe) na magari **5** ni mabovu manne yanasubiri Mnada na moja taratibu la kuanza kuomba kibali cha kuyatoa kwenye Kitabu cha kumbukumbu ya mali za Serikali.

Vile vile kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ina deni la matengenezo ya magari TEMESA Mbeya yenye jumla ya Tsh **29,659,712.50/=** na katika mwaka wa fedha 2021/2022.M

paka tarehe 24/09/2021 Halmashauri imefanya matengenezo yenye jumla Tsh **9,204,118/=** hivyo kufanya deni la TEMESA kufikia **Tshs 38,863,830.50/=**

Inashauriwa deni la TEMESA lianze kupunguzwa kwani kadri siku zinavyozidi kwenda deni linaongezeka.

Jedwali hapo chini linaonesha kila Gari /Pikipiki na hali yake

**A. MAGARI**

| Na | REG NA | MODEL | IDARA | HALI YA GARI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SM 12287 | TOYOTA HILUX D/CABIN | UTAWALA | Linatumika | Liko kwenye hali nzuri/linatumika |
| 2 | SM 12189 | TOYOTA HILUX D/CABIN | UTAWALA | Linatumika | Liko kwenye hali nzuri/linatumika |
| 3 | SM 13106 | TOYOTA TXL PRADO | UTAWALA | Linatumika | Liko kwenye hali nzuri |
| 4 | DFPA 1648 | TOYOTA L/HARD TOP | AFYA TIBA | Nzima | Liko kwenye hali nzuri/linatumika. |
| 5 | Toyota Hilux | STL 9407 | IDARA YA ELIMU MSINGI (EP4R) | Mpya Lilipata ajali. | Gari hili lilipata ajali likiwa linatoka kwenye matengenezo madogo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 21/09/2021 matengenezo ya gari hili yanaendelea |
| 6 | DFPA 6918 | TOYOTA HILUX D/CABIN | AFYA TIBA | Mpya | Liko kwenye hali nzuri/linatumika |
| | SM 12341 | FAW DUMP TRUCK | USAFI/MAZINGIRA | Linatumika | Gari hili linatumika katika shughuli za uzoaji taka. |
| 7 | SM 12342 | FAW DUMP | USAFI/MAZINGIRA | Linatumika | Gari hili linatumika katika shughuli za uzoaji taka. |
| 8 | SM 12679 | Faw Tipper | USAFI/MAZINGIRA | Linatumika | Gari hili linatumika katika shughuli za uzoaji taka. |
| 9 | SM 13790 | TATA BUS | ELIMU MSINGI | Linatumika | Gari hili linatumika kubeba wanafunzi wa shule ya mchepuowa kingereza inayomilikiwa na Halmashauri ya Mji Tunduma |
| 1 | SM 13791 | TATA BUS | ELIMU MSINGI | Linatumika | Gari hili linatumika kubeba wanafunzi wa shule ya mchepuowa kingereza inayomilikiwa na Halmashauri ya Mji Tunduma |
| 1 | STL 1466 | LAND ROVER | TASAF | Limeharibika | Gari hili lilipata tatizo la Engine likiwa linapelekwa TEMESA Mbeya. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1[illegible] | FE517BD-52 | Mitsubishi Canter | UTAWALA | Limeharibika | Gari hili Halmashauri ilipatiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Baada ya kulipeleka temesa kwa ajili ya ukaguzi liligundulika kuwa na tatizo kwenye gear box na nyaraka za matengenezo zinaendelea na matengenezo yataanza mara moja baada ya TEMESA kupewa idhini ya kufanya matengenezo hayo |
| 1[illegible] | SM 8726 | FAW DUMP | USAFI/MAZINGIRA | Halitumiki /Bovu | Gari hili limeondolewa kwenye orodha ya mali za serikali Halmashauri imepewa kibali cha kufanya Mnada wa gari hili. |
| 1[illegible] | SM 8727 | FAW DUMP | USAFI/MAZINGIRA | Halitumiki /Bovu | Gari hili halitumiki na linahitaji matengenezo makubwa vilevile muda wa matumizi umekwisha nashauri taratibu za kuliondoa kwenye daftari la mali za serikali zifanyike |
| | | | | | Gari hili mtumishi ameomba auziwe |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ofisi ya Rais menejimenti ya Utumizi wa Umma |
| 1 | DFP 8990 | TOYOTA HILUX D/CABIN | UTAWALA | Halitumiki /Bovu | Gari hili liliombewa kibali cha kuliondoa kwenye orodha ya mali za serikali ila katibu mkuu wizara ya fedha alitoa maelekezo kuwa gari hili lirudishwe wizarani |
| 17. | SM 11416 | TOYOTA FORTUNER | UTAWALA | Halitumiki /Bovu | Gari hili limeondolewa kwenye orodha ya mali za serikali Halmashauri imepewa kibali cha kufanya Mnada wa gari hili. |

**B. PIKIPIKI**

| NA | REG NO | IDARA | HALI YA PIKIPIKI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | DFPA 2515 | AFYA TIBA - Malaria | Nzima | Inatumika |
| 2. | DFPA 1496 | AFYA TIBA-Chanjo | Imeharibika | Haitumiki inahitaji matengenezo ya Engine |
| 3. | DFPA 3170 | U/MAZINGIRA | Imeibiwa | Taarifa ya kuibiwa ipo kwenye file la mtumishi Pius Simbee wa Idara ya Afya. Iliibiwa tarehe 1 August 2020 RB No. TDM/IR/1604/2021. Uchunguzi unaendelea |
| 4. | STL 5516 | U/MAZINGIRA | Nzima | Inatumika Utawala |
| 5. | DFPA 4702 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7. | DFPA 5254 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |
| 8. | DFPA 5248 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |
| 9. | DFPA 5245 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |
| 10. | DFPA 4783 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |
| 11. | DFPA 4754 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |
| 12. | DFPA 4773 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |
| 13. | DFPA 4710 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |
| 14. | DFPA 4774 | ELIMU MSINGI | Imeharibika | Inahitaji kufanyiwa matengenezo ya Engine na kufungwa tairi mpya |
| 15. | DFPA 5246 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |
| 16. | DFPA 4701 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |
| 17. | DFPA 4970 | ELIMU MSINGI | Nzima | Inatumika |
| 18. | DFPA 4755 | ELIMU MSINGI | Imeibwa | Taarifa ya kuiba ipo kwenye file la Afisa Elimu aliyekabidhiwa ndugu Agustino Mwang'onda. Iliibiwa tarehe 10 March 2019 ilifunguliwa jalada Polisi kwa namba RB No.<br>MPB/IR/112/2019<br>Uchunguzi unaendelea. |
| 19. | SM 13160 | MIFUGO | Nzima | Inatumika |
| 20. | SM 13161 | MIFUGO | Nzima | Inatumika |
| 21. | SM 13162 | KILIMO | Nzima | Inatumika |
| 22. | SM 13594 | KILIMO | Nzima | Inatumika |
| 23. | SM 13595 | KILIMO | Nzima | Inatumika |
| 24. | SM 13596 | KILIMO | Nzima | Inatumika |
| 25. | SM 13597 | UJENZI | Nzima | Inatumika |
| 26. | SM 13598 | UJENZI | Nzima | Inatumika |
| 27. | SM 13599 | KILIMO | Nzima | Inatumika |

**C. MAFUTA**

jumla ya mafuta lita **56682** kwa ajili ya Miradi, Idara na Vitengo kama ifuatavyo;

- Utawala lita 20000
- Mazingira lita 16000
- Ujenzi lita 2000
- Afya 3700
- Kituo cha Afya Chiwezi 2818
- Kituo cha Afya Chipaka 1700
- Elimu Msingi lita 1400
- English Medium 5000
- Elimu sekondari 847
- Maporomoko lita 500h
- Jengo la Utawala lita 2717

Wajumbe waliipokea taarifa ya Magari,Mafuta na Pikipiki katika kipindi cha kuishia tarehe 30 Septemba 2021 na kushauri iwasilishwe katika kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala.

**MUHT. NA.TTC/CMT/09/10/2021 MAPENDEKEZO NA USHAURI KUHUSU UTOAJI WA MIKOPO KWA VIKUNDI YENYE TIJA**

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii aliwasilisha taarifa kuhusu mapendekezo ya utoaji wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake,Vijana na Wenye Ulemavu.

Ilielezwa kwamba Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 kwa kanuni zilizotungwa chini ya kifungu 37(A) na kutolewa katika Tangazo la Serikali Na 286 la Tarehe 5/4/2019 pamoja na marekebisho ya kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu liliyotolewa kwenye Tangazo la Serikali Na. 217 la Tarehe 26/02/2021, pamoja na mwongozo wa usimamizi wa Fedha za uendeshaji Akaunti ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa Halmashauri (Machi 2020).

Mfuko huu wa Maendeleo ya Wanawake,Vijana na watu wenye Ulemavu ni Mfuko wa Mzunguko na endelevu na upo kwa mujibu wa Sheria za uendeshaji Mamlaka za Serikali za Mitaa unaohusika na utengaji wa fedha kwa asilimia 10% kwa ajili ya kuwezesha vikundi kiuchumi kwa kutoa mikopo kwa vikundi kwa mgawanyo 4% wanawake, 4% Vijana na 2% watu wenye Ulemavu unaotakana na makusanyo ya mapato ya ndani.

## CHIMBUKO LA MAPENDEKEZO

Mapendekezo haya yanawasilisha kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa katika vikao kazi kwa viongozi wa Jumuiya ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika vikao vilivyofanyika Jijini Dodoma mwishoni mwa mwezi Septemba 2021.

Mheshimiwa Rais na Wah.Mawaziri wenye dhamana wa Ofisi ya OR-TAMISEMI kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha wanaendelea kutenga 10% ya mapato ya ndani na kutoa mikopo yenye Tija kwa vikundi vya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu,Na kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa ziache kutoa mikopo midogo midogo kwa vikundi ambayo hata kama kikundi kinakuwa kimekamilisha marejesho ya Mkopo kwa wakati wanabaki bila Mafanikio au mabadiliko yoyote ya ukuaji wa uchumi, mitaji au faida yoyote ile inayopelekea vikundi vingi kutoonyesha mafanikio chanya ya fedha zilizokopeshwa.

## MAPENDEKEZO YA MAKUBALIANO YA UTEKELEZAJI

i. Halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii kuendelea kuhamasisha uundwaji wa vikundi, kutambua vikundi mbalimbali vyenye mtazamo wa uwekezaji pamoja na kuvisajili.

ii. Halmashauri kupitia Idara za Sekta za uzalishaji,usafirishaji na ujenzi kuwa sehemu ya kuibua makundi na kuwajengea ushawishi wa kuunda vikundi vya kiuchumi kwa mujibu wa mwongozo kwa kushirikiana na wataalam wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii.

iii. Kutoa kipaombele cha utoaji wa mikopo kwa vikundi vyenye mtazamo wa uwekezaji, viwanda, usafirishaji na ujenzi kwa kuwawezesha vifaa au vitendea kazi na siyo kupewa fedha taslimu.

    *Rejea Mwongozo wa usimamizi wa Fedha za uendeshaji Akaunti ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa Halmashauri uliotolewa na OR-TAMISEMI (Machi 2020). Sehemu ya pili kifungu 2.6.3 inayoelekeza Halmashauri inaweza kununua moja kwa moja kifaa au vifaa na kuvitoa kwa kikundi au vikundi na kutambuliwa kama sehemu ya mkopo kwa kikundi kwa kwa makubaliano maalum na kikundi kuwa maombi hayo ya vifaa yameombwa na kikundi na kuridhiwa thamani ya gharama ya manunuzi pamoja na muda maalum wa kuanza kufanya marejesho.*

iv. Kuwezesha vikundi vya kisekta kuanzisha miradi kwa kuongeza mnyororo wa thamani ,Kama vile uanzishaji wa miradi ya mashine za uchakataji nafaka,usindikaji ,upangaji madaraja na ufungashaji.

v. Halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii kuviunganisha vikundi vyenye mwelekeo wa aina moja ya shughuli kuunda Umoja wa vikundi hivyo na kuwezesha

vidogo vidogo vya sekta husika. ***Mfano:*** utengenezaji wa sabuni za miche na maji ,utengenezaji Batiki na ununuzi wa samaki.

Wajumbe waliridhia mapendekezo ya utoaji wa Mikopo yenye tija kwa kuongeza viwango ili kiuchochea uchumi na ajira kwa Vijana na kwamba taarifa iwasilishwe katika kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala.

**MUHT. NA.TTC/CMT/10/10/2021 MAPENDEKEZO YA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA AJILI YA UJENZI WA MAJENGO YA GHOROFA KATIKA SHULE ZA MSINGI**

Ilielezwa kwamba Halmashauri ya Mji Tunduma kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ilipanga kujenga madarasa kwa shule ya msingi na shule ya sekondari kujengwa kwa ghorofa.
Hii ni kwa sababu ya changamoto zifuatazo:-

1. Ukosefu wa maeneo ya kutosha kujenga shule kulingana na ongezeko la watu katika Halmashauri.
2. Kuanza kujenga miundombinu ya kisasa ili kuuwezesha mji kuwa katika hali ya kupendeza.

Kwa sasa Halmashauri inataka kujenga vyumba vya madarasa ya ghorofa katika shule ya msingi Haisoja kwa vyumba 10 linakadiriwa kugharimu Tshs 600,000,000 ambapo fedha hizi zitapatikana kwa kuhahirisha baadhi ya miradi ili kupisha mradi huu.
Naleta katika kikao hiki kupata ridhaa ya kuanza kujenga vyumba vya madarasa kwa ghorofa katika maeneo mbalimbali ambayo yanaupungufu wa ardhi na wingi wa watoto.
Baada ya kuwasilisha taarifa wajumbe waliipokea na kuridhia mfumo wa ujenzi wa Majengo ya Taasisi kwa ramani za Ghorofa ambapo kwa kuanzia ilipendekezwa Shule ya Msingi Haisoja iliyopo katika Kata ya Sogea.

Mhe.Makamu Mwenyekiti alipongeza na kwamba Mpango huu ni mzuri iwapo utafanikiwa.

Mhe.Kwintin Kayombo alipongeza na kushauri utekelezaji uanze mapema.Aidha alitaka kujua maeneo yanayopendekezwa kwa ajili ya ujenzi wa Shule za ghorofa na chanzo chake cha fedha.

**Jibu:** Ilielezwa kwamba Mpango huu utatekelezwa katika maeneo mbalimbali hasa yenye ukosefu wa maeneo tukianzia na Shule ya Msingi Haisoja.

Kuhusu chanzo cha fedha ilielezwa kwamba ni mapato ya ndani ambapo kwa kuanzia kuna fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 40 vya madarasa.

hasa katika maeneo yenye uhaba wa maeneo kwa ajili kujenga vyumba vya madarasa.

Wajumbe walipitisha Mfumo wa Ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ramani za Ghorofa.

**MUHT.NA.TTC/CMT/11/10/2021 USIMAMIZI WA TAKA NGUMU KATIKA KATA 3 ZA MAJARIBIO**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira aliwasilisha taarifa kuhusu Mpango wa majaribio wa usimamizi wa makusanyo ya uzalishaji wa taka ngumu katika Kata **3** ambazo ni Majengo,Tunduma na Mpemba.

Ilielezwa kwamba kabla ya kuanza kubadilisha mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa huduma ya uondoshaji wa taka katika Mitaa na Kata, imependekezwa kuanza na Kata chache ambazo ni Mpemba,Tunduma na Majengo.

Aidha fedha zote zitakazokusanywa zitaingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri ili kufanya tathmini kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi kwa kuzingatia makisio ya ukusanyaji wa mapato kama mchanganuo unavyooneshwa kupitia jedwali

**Jedwali 1: Idadi ya Kaya na maeneo ya biashara ngazi ya Kata**

| Na | Jina la Kata | Jina la Mtaa | Idadi ya kaya | Idadi ya Biashara | Makisio ya makusanyo ya kaya kwa mwezi | Makisio ya makusanyo ya kaya kwa mwaka | Makisio ya makusanyo ya biashara kwa mwezi | makisioyamakusanyobiasharakwamwaka |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MPEMBA | Sefu | 966 | 175 | 966,000 | 11,592,000 | 875,000 | 10,500,000 |
| | | Kokoto | 490 | 48 | 490,000 | 5,880,000 | 240,000 | 2,880,000 |
| | | Nansele | 773 | 51 | 773,000 | 9,276,000 | 255,000 | 3,060,000 |
| | | Mpemba | 863 | 161 | 863,000 | 10,356,000 | 805,000 | 9,660,000 |
| | | Katenjele | 213 | - | | - | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Nandanga | 407 | - | | - | | |
| | **Jumlandogo** | **7** | **4,051** | **435** | **3,092,000** | **37,104,000** | **2,175,000** | **26,100,000** |
| | | **JUMLA** | | | **63,204,000** | | | |
| **2** | **TUNDUMA** | Unyamwanga | 367 | 200 | 367,000 | 4,404,000 | 1,000,000 | 12,000,000 |
| | | Tundumakati | 167 | 1,248 | 167,000 | 2,004,000 | 6,240,000 | 74,880,000 |
| | | Ihanda | 361 | 9 | 361,000 | 4,332,000 | 45,000 | 540,000 |
| | | Sikanyika | 99 | 1,383 | 99,000 | 1,188,000 | 6,915,000 | 82,980,000 |
| | | Tukuyu | 195 | 76 | 195,000 | 2,340,000 | 380,000 | 4,560,000 |
| | **Jumla ndogo** | 5 | **1,188** | **2,916** | **1,188,000** | **14,268,000** | **14,580,000** | **174,960,000** |
| | | | **JUMLA** | | | **189,228,000** | | |
| **3** | **MAJENGO** | Majengo A | 737 | 155 | 737,000 | 8,844,000 | 775,000 | 9,300,000 |
| | | Majengo B | 627 | 60 | 627,000 | 7,524,000 | 300,000 | 3,600,000 |
| | | Majengo C | 730 | 119 | 730,000 | 8,760,000 | 595,000 | 7,140,000 |
| | | MajengoMapya | 2982 | 359 | 2,982,000 | 35,784,000 | 1,795,000 | 21,540,000 |
| | **Jumla ndogo** | **4** | **5,076** | **693** | **5,076,000** | **60,912,000** | **3,465,000** | **41,580,000** |
| | | | **JUMLA** | | | **102,492,000** | | |
| | | | **JUMLA KUU MPEMBA+TUNDUMA+MAJENGO 354,924,000** | | | | | |

Baada ya kuwasilisha taarifa wajumbe waliipokea na kuijadili kama ifuatavyo;-

Wajumbe walipitisha Mfumo wa usimamizi wa makusanyo na uzoaji wa taka ngumu katika Halmashauri ya Mji Tunduma kwa kuanzia na Kata ya Majengo,Tunduma na Mpemba na kushauri kabla ya kuanza utekelezaji taarifa iwasilishwe katika kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala.

**MUHT.NA.TTC/CMT/12/10/2021 MAPOKEZI YA FEDHA KWA AJILI YA MRADI WA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19**

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2021 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa kiasi cha **Tshs 1,880,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali kupitia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19 katika Halmashauri yetu.

Miradi itakayotekelezwa ni ;-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa vyumba 52 vya madarasa @ 20,000,000 = | 1,040,000,000 |
| 2. | Shule Shikizi ya Benzuma @20,000,000 = | 40,000,000 |
| 3. | Bweni la Mahitaji maalum Tunduma SM | 80,000,000 |
| 4. | Jengo la dharula | 300,000,000 |
| 5. | Mtambo wa X- Ray | 420,000,000 |
| | **JUMLA** | **1,880,000.00** |

Wajumbe waliridhia utekelezaji wa miradi kupitia Mradi wa Ustawi wa Taifa kupitia Mapambano dhidi ya UVIKO-19

**MUHT. NA.TTC/CT/13/10/2021 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

**-Hakuna**

**MUHT. NA.TTC/CMT/14/10/2021 KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kufunga kikao, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kujadili taarifa kwa umakini.Aliwataka kila mmoja kutekeleza wajibu wake kikamilifu.Kisha alifunga kikao mnamo saa **09:50** jioni.

**UMETHIBITISHWA** na kusainiwa na;

| | | |
|---|---|---|
| ……………………………… | …/…/20.. | ……………………………… |
| Ndg.Philemon M.Magesa | **TAREHE** | Ndg.Josephat W.Kayombo |
| **MWENYEKITI** | | **KATIBU** |